

TAARIFA KWA WASAFIRISHAJI WA NAFAKA NA MAZAO MCHANGANYIKO KUHUSU UTARATIBU WA KUOMBA VIBALI VYA KUSAFIRISHA MAZAO NJE YA NCHI



#ShirikishaBoreshoEndeleza

1

Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko (COPRA), inapenda kuwajulisha wasafirishaji wote wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko kuwa, kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo imeboresha mfumo wa maombi ya vibali kutoka ATMIS kwenda eKilimo. Maboresho hayo yalianza tangu tarehe 14 Desemba 2024 ambapo mfumo wa eKilimo ndio mfumo rasmi wa kutoa vibali hivyo.

2

Mamlaka inawajulisha na kuwasisitiza wasafirishaji wote kuendelea kufanya maboresho ya akaunti zao kwa kujisajili upya kuitia ujumbe wa barua pepe uliotumwa kwenye barua pepe zao. Maombi yote ya vibali yatumwe kwenye mfumo mpya ulioboreshwa wa e-Kilimo.

3

Aidha, wasafirishaji ambao hawakuwahi kujisajili katika mfumo wa ATMIS wanaweza kujisajili upya katika mfumo mpya ulioboreshwa wa e-Kilimo (<https://portal.kilimo.go.tz/>) kwa kubonyeza neno 'Register'

4

Kwa maelezo zaidi piga simu namba +255714605155 au tembelea Tovuti www.copra.go.tz